# CROWN EXAMINATION TEST
# MUHULA WA TATU - 2021
## DARASA LA SITA: KISWAHILI

Muda: Saa 1 dakika 40

**Kifungu kifuatacho kina nafasi 1 - 15. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliopewa kujazia nafasi zilizoachwa wazi.**

Ni dhahiri ___1___ kuwa ili ___2___ dhifa fulani pamoja na wengi ni ___3___ upokee ___4___. Vivyo hivyo ili uingie katika mbuga ___5___ wanyama ___6___ ile ni lazima ulipe ___7___ kishà ukabidhiwe ___8___ ambayo utaitumia kama ___9___ ya kulipa. Baada ya hapo, ndipo sasa utakuwa na ___10___ ya kuingia ndani ili ___11___ wanyama. Humo ___12___ wanyama wengi ___13___ ndovu, kifaru, simba na chui. ___14___ utawaona nyuni wengi, si tausi, mbuni, si kanga ___15___ korongo.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | shayiri | shairi | shariri | shahiri |
| 2. | usherehe | usheherehekee | usheherekee | usherekee |
| 3. | shati | sharuti | bora | sharti |
| 4. | mwaliko | kadi | risiti | ujumbe |
| 5. | ya | la | kwa | pa |
| 6. | lolote | yeyote | yoyote | popote |
| 7. | ada | koto | arbuni | kiingilio |
| 8. | tikiti | karatasi | tiketi | fimbo |
| 9. | udhibitisho | ithibati | idhibati | ishara |
| 10. | nia | akili | furaha | ruhusa |
| 11. | kuwatazama | kuwaona | kuwaangalia | kuwatumbulia |
| 12. | nitawaona | utawaona | tutawaona | mtawaona |
| 13. | fauka | licha | mithili | kama |
| 14. | Aidha | Hasahasa | Ata | Kisha |
| 15. | hadi | ata | sisemi | si |

**Kuanzia swali la 16 - 30, jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa**

16. Malipo kwa ajili ya hasara huitwaje?
   A. Ridhaa
   B. Fidia
   C. Sadaka
   D. Koto
17. Kandarasi ni
   A. aendeshaye garimoshi
   B. makubaliano ya kazi ya muda fulani
   C. Mauzo ya bidhaa kwa kushindania bei
   D. Malipo baada ya kustaafu kazi
18. Saa nne kasoro ni
   A. 3 : 45
   B. 4: 15
   C. 9: 45
   D. 10 : 15
19. Mtoto wa ngamia huitwaje?
   A. Kimatu
   B. Buu
   C. nirihi
   D. kiluwiluwi

20. Neno lipi halifai kwenye orodha hii?


A. Heroe

B. Kipanga

C. Mjusi

D. Shomoro

21. Vazi hili linajulikana kama



A. bombo

B. suruali ndefu

C. kachiri

D. shati

22. Ukitaka mtu akupishe njia utamwambiaje?

A. Ebu!

B. Simile!

C. Ketle!

D. Abee!

23. Ni upi umoja wa

Makazi haya hayapendezi

A. Kazi hii haipendezi

B. Makazi haya haipendezi

C. Kazi hili halipendezi

D. Makazi haya hayapendezi

24. Mwana aliyefiwa na wazaziwe huitwa vipi?

A. Mjane

B. Yatima

C. Mwanamkiwa

D. Kiokote

25. Majira ya mvua kubwa huitwa

A. mchoo

B. masika

C. kifuku

D. vuli

26. Nini wingi wa

Wembe huu ni butu haukati

A. Mawembe haya ni mabutu hayakati

B. Nyembe hizi ni butu hazikati

C. Viwembe hivi ni vibutu havikati

D. Wembe hii ni butu haikati

27. Jumba la wahindi la kuabudia huitwaje?


A. Maabadi

B. Sinagogi

C. Hekalu

D. Msikiti

28. Kifaa hiki cha ufundi hujulikana kama



A. nyundo

B. pasi

C. msumeno

D. shepe

29. Tumia kiashiria kisisitizi

Nitasoma kitabu __________

A. hiki hiki

B. iki hiki

C. kiki hiki

D. kiki kiki

30. Unda kitenzi kutokana na nomino "mpishi"

A. pika

B. pikika

C. mpikaji

D. chakula

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Mambo aliimbuka kuwa <u>nguli</u> masomoni. Tangu darasa la kwanza hadi la nne hakudiriki kuwahi nambari nyingine ila namba moja. Walimu walimhimiza aongeze ari masomoni naye kwani hakuwa sikio la kufa, akayapokea mawaidha hayo kwa mikono miwili. Taabu aliyoikabili ilimwimarisha badala ya kumdhalilisha. Alielewa peupe kuwa masomo ndiyo yalikuwa silaha bora zaidi ya kuupiga <u>uchochole</u> ulioiparamia aila yao kama goromwe auparamiavyo mti aonapo hasimu. Waama, alinga'amua kinaganaga bin kinagaubaga kuwa elimu ndiyo daraja livushalo toka ng'ambo ya ulalahoi hadi ile ya donge nono.

Baada ya miaka minane ya kudurusu. Mambo aliukalia mtihani, naye akatia fora wee! Aliibuka gwiji kidedea katika mudiria mzima. Matokeo yake yaliwashangaza wengi. Kweli, kuinamako ndiko kuinukako na usione wembamba wa reli ukaidharau kwani garimoshi hupita juu.

31. Neno lipi halina maana sawa na <u>nguli</u>?
A. Gwiji
B. Mahiri
C. Mbuji
D. Bunga

32. Kinyume cha <u>uchochole</u> ni
A. umaskini
B. utajiri
C. ukwasi
D. ufukara

33. Kutoka darasa la kwanza hadi la nne _______
A. Mambo hakukosa kuwa nambari moja
B. Mambo hakuwahi kuwa nambari moja
C. Mambo alijaribu kuwa nambari moja
D. Mambo hakujaribu ili awe nambari moja

34. "<u>Walimu walimhimiza</u>" ..... yaani _______
A. walimtia moyo
B. walimvunja moyo
C. walimkatisha tama
D. angeongeza ari masomoni

35. Kama Mambo angekuwa sikio la kufa _______
A. angeyapokea mawaidha
B. asingeyapokea mawaidha
C. angeyazingatia mawaidha
D. angeongeza ari masomoni

36. Kipi hakikumfanya mambo atie bidii masomoni?
A. Mawaidha aliyoyapata
B. Shida alizozipata
C. Kuithamini elimu
D. Kukosa matumaini

37. "................... <u>ulioparamia aila yao kama nguruwe</u>."
Hii ni fani gani ya lugha?
A. Msemo
B. Tashbihi
C. Istiara
D. Nahau

38. Baada ya Mambo kuukalia mtihani _______
A. alifua dafu
B. alipiga moyo konde
C. alikula mwande
D. alishika mkia

39. Kwa nini matokeo ya Mamboyaliwashangaza wengi?
A. Hakuwa mwerevu shuleni
B. Walitarajia angefaulu
C. Walidhani shida ingemzuia asifanye vyema
D. Walimwonea wivu

40. Methali ipi inalingana na ufahamu huu
A. Haraka haraka haina baraka
B. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
C. Haba na haba hujaza kibaba
D. Pole pole ndio mwendo

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 - 50.</u>***

Mbuzi ni miongoni mwa wanyama ambao yawezekana wafugwe kwa gharama ndogo sana. Mbali na kuwa katika kategori ya wanyama walio na uwezo wa kustahimili mabadiliko mbalimbali ya hali ya hewa, mbuzi huzaana kwa haraka sana.

Wafugaji wengi wa mbuzi hujipata wakiwa na zizi kubwa chini ya kipindi kifupi cha muda hasa iwapo watakumbatia ufugaji wa mbuzi wenye uwezo wa kukopoa zaidi ya wanambuzi wawili kwa pamoja. Ili kutambua mbuzi mwafaka wa kumfuga, makini zaidi yastahili kuelekezwa kwa rangi ya wanyama hao kwa kuwa ndicho kigezo cha kutathmini uwezo wao wa kuhimili mabadiliko mbalimbali ya hali ya hewa.

Iwapo lengo la kuwafuga mbuzi ni kwa misingi ya nyama au maziwa pekee, basi uwezo wa mbuzi husika wa kukabiliana na magonjwa ya aina mbalimbali ni sifa muhimu sana ya kuzingatia kabla ya kujitosa katika ufugaji huu. Mzee Moses Wanderi ni mfugaji maarufu kutoka eneo la Marugoine, viungani mwa milima ya Dundori, kaunti ya Nakuru. Mnamo 2013 alianzisha mradi wa kuwafuga mbuzi akitumia mtaji wa 3,000 pekee zilizotokana na akiba ya muda mfupi. Alikusudia kuwafunulia vijana kuhusu tija iliyomo

katika ukulima na ufugaji wa wanyama wadogowadogo badala ya kutegemea kazi za kuajiriwa ambazo kwa sasa ni nadra sana kupatikana.

Bw. Wanderi anasema kazi ya kujiajiri ni bora zaidi kuliko ile ya kuajiriwa kwa sababu kila mfugaji au mkulima hujisakia riziki kutokana na jasho lake mwenyewe na kujiongezea kipato kutokana na mahitaji ya soko bila ya kutegemea serikali impatie ajira. Akimiliki jumla ya mbuzi 15 kufikia sasa, Bw. Wandera alisimulia **Akilimali** kwamba yeye hulazimika kuhifadhi kumbukumbu za uzalishaji kila mwezi ili kufuatilia mazao katika shamba lake dogo ambalo ameliteua mahsusi liwe la kuwafungua mbuzi. Mpangilio huo umemwezesha Bw. Wanderi kupata mikopo pamoja na kuhudhuria warsha na makongamano ya ushauri nasaha kuhusu mbinu mwafaka zaidi za ufugaji bila ya kufuata mikondo mirefu ya kuchosha.

41. Kulingana na aya ya kwanza, mbuzi
 A. huzaana kwa haraka sana
 B. ni mnyama mvivu sana
 C. ni mnyama asiye na manufaa yeyote
 D. si mnyama mwenye faida

42. Kulingana na makala haya, mbuzi huishi wapi
 A. kwenye pango
 B. kwenye zizi
 C. kwenye kizimba
 D. kwenye zeriba

43. Kikembe cha mbuzi ni
 A. ndama
 B. shibli
 C. mwanambuzi
 D. kimatu

44. Kulingana na makala haya, faida za mbuzi ni
 A. nyama, maziwa na mapato
 B. nyama, ngozi na mayai
 C. mayai, nyama na maziwa
 D. nyama, maziwa, na hasara

45. Kulingana na mzee Wanderi
 A. kilimo hakina faida
 B. afadhali kazi ya kuajiriwa
 C. kazi ya kujiajiri ni bora kuliko kuajiriwa
 D. vijana hawafai kufanya ukulima

46. Kisawe cha neno ajira ni
 A. pesa
 B. kazi
 C. mbuzi
 D. ukulima

47. Nomino 'mbuzi' iko kwenye ngeli gani
 A. LI - YA
 B. A - WA
 C. KU - KU
 D. U - YA

48. Mzee wanderi hufuatilia uzalishaji wa mbuzi wake vipi?
 A. Yeye huweka kumbukumbu za ushalishaji wa mbuzi wake
 B. Mkwewe humkumbusha
 C. Yeye huwepa kumbukumbu katika tarakilishi
 D. Yeye hukumbuka tu bila kuweka kumbukumbu

49. Ni mnyama yupi wa porini anayefanana na mbuzi
 A. kima
 B. paa
 C. kondoo
 D. mbogo

50. Kichwa mwafaka kwa makala haya ni
 A. Ukulima
 B. Faida za mbuzi wa kiasili
 C. Faida za mifugo
 D. Kumbukumbu za mzee Wanderi